




www.womenonwaves.org
www.womenonweb.org

Women on Waves: Kujifungua Kwa Njia Ya Usalama Ukitumia Misoprostol

Misoprostol yaweza kuzuia kupoteza damu kwa wingi ukeni baada ya kujifungua, kwa lugha ya kimombo, (postpartum hemorrhage).


Hivi ndivyo unavyoweza kuitumia kwa njia ya usalama.



2.

Ndani ya dakika MOJA baada ya mtoto kuzaliwa:


Papasa tumbo ili kukagua kama hakuna mtoto mwagine, yaani mapacha.



4.

Dakika tatu baada ya kujifungua:

Funga kamba ya kitovu ukitumia nyuzi mbili safi kabla ya kukata kamba ya kitovu ukitumia wembe mpya na ngojea mfuko wa mimba kutoka.



1.


Mara tu baada ya kujifungua:

Mkaushe mtoto kisha mlaze juu ya tumbo la mama. Funika mtoto kwa nguo ya joto au blangeti.

3.

Ndani ya dakika MOJA baada ya mtoto kuzaliwa:


Weka vidonge vitatu vya Misoprostol (kila tembe moja 200mcg) chini ya ulimi wa mama aliyejifungua ili kuleta machungu. Ziwache zitulie angalau kwa nusu saa kabla ya kuzimeza.



5.

Baada ya mfuko wa mimba kutoka:

Kanda tumbo kuanzia juu baada ya mfuko wa mimba kutoka hadi tumbo lirudi kuwa kama mpira mgumu. Fanya hivi kila baada ya dakika 15 kwa kipindi cha masaa mawili yanayofuata.



NENDA HOSPITALINI KWA HARAKA KAMA:

Mfuko wa mimba haujatoka ndani ya dakika 30

au

Mwanamke kuanza au kuendelea kutokwa na damu nyingi baada ya kutumia Misoprostol



Kwa taarifa zaidi, nenda kwa www.womenonwaves.org au tuma barua pepe kwa info@womenonweb.org